JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA

MAZUNGUMZO YA WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA NA WAANDISHI WA HABARI, KUHUSU HALI YA KILIMO NA USHIRIKA NCHINI TAREHE 08 JANUARI, 2008

1. UMUHIMU WA SEKTA YA KILIMO

Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 45 ya pato la Taifa, asilimia 30 ya pato la kigeni; kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania na kuzalisha zaidi ya asilimia 95 ya chakula kinachotumika hapa nchini.

Tanzania ina eneo la hekta milioni 43 zinazofaa kwa kilimo, kati ya hizo ha. 10.8 milioni ndizo zinazolimwa.

2. Pamoja na mchango mkubwa wa kilimo katika uchumi wa Taifa, jamii ya wananchi waishio vijijini bado inakabiliwa na umasikini wa kipato.

3. Sababu za hali hii zimefafanuliwa vizuri katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama ifuatavyo:-

Kilimo ndio msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika modernization ya uchumi wa Tanzania. Kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga uchumi wa kisasa. **Lakini** kilimo cha Tanzania kina matatizo yafuatayo:

(a) Wakulima walio wengi hawazijui na hawazitekelezi Kanuni za kilimo bora za mazao wanayolima, hivyo kilimo chao hakina tija na mavuno yao ni kidogo.

(b) Wakulima wetu kwa wastani, wanalima vishamba vidogo vidogo.

(c) Wakulima wetu wanategemea zana duni za jadi hasa jembe la mkono.

(d) Upatikanaji wa mbegu bora na mbolea haujawa na mfumo wa uhakika na matumizi yake hayajaenea kwa wakulima.

(e) Karibu kazi zote za kilimo, zinategemea nguvu kazi hasa ya wanawake.

(f) Maji ya mvua yanaendelea kuachwa yaende baharini, badala ya kuyakinga kwenye visima, malambo na mabwana, kwa matumizi ya watu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

4. Wajibu wa Serikali ya Awamu ya Nne.

Katika kuendeleza Sekta ya Kilimo, Serikali ya awamu ya nne ina wajibu wa kubadilisha hali iliyoelezwa hapo juu, ili kuweka mazingira ambayo wananchi (wakulima) wataongeza tija katika kilimo chao, wataongeza kipato chao kupunguza kiwango cha umasikini na hivyo kujiletea maisha bora.

Serikali kwa kutambua nafasi ya sekta ya kilimo katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini na katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, imetayarisha Program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, ***Agriculture Sector Development Programme (ASDP)*** ambayo imeanza kutekelezwa mwaka 2006/07 na Wizara nne zinazohusika na Sekta ya Kilimo yaani Kilimo, Mifugo, Viwanda na Tawala za Mikoa. Program imekadiriwa kugharimu shillingi 2.5 trillion katika kipindi cha miaka saba, (2006/07 – 2012/13). Program hii inagharimiwa na Serikali pamoja na wafadhili kupitia mfuko wa pamoja yaani (ASDP Basket Fund).

5. Malengo Makuu ya ASDP

I. Kuwezesha wakulima na wafugaji kuongeza tija na uzalishaji ili kupata faida na mapato, kwa kuwapatia elimu, teknolojia, miundo mbinu na masoko ya uhakika.

II. Kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo kwa kujenga mazingira bora ya kisera na kisheria.

6. Ngazi za Utekelezaji wa Program

Utekelezaji wa Program unafanyikia katika ngazi kuu mbili.

(1) Ngazi ya Wizara Kitaifa.

(2) Ngazi ya Wilaya na Vijiji.

Utekelezaji katika ngazi ya Taifa ni jukumu la Wizara za Sekta ya Kilimo ikiwemo Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Shughuli zinazotekelezwa zinagawanyika katika maeneo yafuatayo:-

(i) Huduma za kilimo (utafiti na ugani)
(ii) Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji.
(iii) Uendelezaji masoko wa sekta binafsi.
(iv) Uhakika wa upatikanaji wa chakula.
(v) Uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

Huduma hizi za kitaifa zina maana tu kama zinawafikia walengwa yaani wakulima. Kwa mantiki hiyo, utekelezaji halisi wa Program ya ASDP unatekelezwa zaidi katika ngazi ya wilaya na vijiji ambako ndiko walengwa waliko.

7. Utekelezaji wa Sekta ya Kilimo, ngazi ya Wilaya na Vijiji

Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo wilayani na Vijijini unachangiwa na wadau mbalimbali kupitia mipango ya maendeleo ya wilaya ***District Agricultural Development Plans (DADPs).*** Wadau hao ni pamoja na wakulima wenyewe, Serikali za Mitaa, asasi zisizo za kiserikali na sekta binafsi. Utekelezaji wa program ngazi ya wilaya ni jukumu la Serikali za Mitaa, chini ya uangalizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kutokana na umuhimu wa ngazi hii ya utekelezaji wa Program, asilimia 75 ya raslimali za Program zinatumika ngazi ya wilaya na vijiji vilivyo na mipango.

Mipango ya DADPs ina maeneo makuu matatu ya utekelezaji, na ruzuku zinatolewa na Serikali kwa kuzingatia maeneo hayo kama ifuatavyo:-

(i) Uwekezaji katika miradi ya kuendeleza kilimo wilayani, unapewa ruzuku ya uwekezaji.

(ii) Uboreshaji wa huduma za kilimo unapewa ruzuku ya kuboresha huduma za kilimo.

(iii) Kujenga uwezo wa utekelezaji wa mipango kwa watendaji na wakulima na kuboresha mifumo ya utendaji inapewa ruzuku ya kujenga uwezo wa wakulima na Serikali za Mitaa kuboresha mifumo ya utendaji.

Mbali na DADPs, pia iko miradi ya maendeleo ***(Area Based)*** ambayo ilishaanza na inaendelea kutekeleza miradi ambayo ni sehemu ya ASDP. Miradi hiyo ni pamoja na;

(i) ***Participatory Agricultural Development Project (PADEP)*** ambao unatekelezwa katika mikoa 10 ya Morogoro, Tanga, Tabora, Singida, Lindi, Mtwara, Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Ruvuma.

(ii) ***Agricultural Sector Programme Support (ASDS)*** ambao unatekelezwa katika mikoa 2 ya (Iringa na Mbeya) na;

(iii) ***District Agricultural Sector Investment Project (DASIP)*** ambao unatekelezwa katika mikoa mitano ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kigoma na Kagera.

Miradi yote hii inawekeza katika miradi inayoibuliwa na wananchi wenyewe, na ambayo wananchi wenyewe wanachangia nguvu zao na sehemu ya mali zao. Miradi ya PADEP, ASPS**,** na *DASIP* iko mahali pengi huko wilayani. Maeneo yanayohudumiwa na miradi ya PADEP na ASDS iliyoanza mapema zaidi imeonyesha mafanikio. Ziko familia ambazo

zimeongeza kipato chao kupitia miradi hii, na pia kuna huduma za kilimo na mifugo kama vile umwagiliaji, majosho na mabwawa yaliyojengwa chini ya miradi hii.

Maeneo Yaliyopewa Kipaumbele Katika Kutekeleza ASDP Pamoja na Utekelezaji wake ni kama Ifuatavyo:

8. Kujenga Uwezo wa Halmashauri za Wilaya na Vijiji

- Miongozo ya kupanga, kutekeleza, kusimamia, kutathmini na kufuatilia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) imetayarishwa na kusambazwa katika Halmashauri zote za wilaya na Mikoa.
- Mafunzo ya kujenga uwezo wa kuandaa, kutekeleza na kutathimini (DADPs) yametolewa kwa Halmashauri zote na Sekretariati za mikoa kwa Maofisa zaidi ya 1,062.
- Halmashauri 132 zilijengewa uwezo wa kuandaa DADPs kwa mwaka 2007/2008;
- Kuelimisha na kuhamasisha viongozi wa ngazi mbalimbali katika Serikali kuhusu ASDP;
- Mfumo wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa ASDP umeandaliwa na umeanza kujaribiwa katika maeneo mbalimbali nchini.

9. Kuhimiza Sekta Binafsi Kushiriki katika Kilimo

- Wizara imekuwa ikishirikisha asasi za sekta binafsi na zisizo za kiserikali katika warsha, mafunzo yatakayoziwezesha kushiriki kikamilifu katika kutekeleza ASDP. Watoa huduma 318 wa sekta binafsi walipatiwa mafunzo mbalimbali.
- Taasisi binafsi za utafiti zimewezeshwa kwa kupatiwa fedha ili kutekeleza ASDP (TRIT, TaCRI na TORITA).
- Sekta binafsi inashiriki katika kujenga miundombinu ya kilimo, kutoa huduma za kusambaza na kuuza pembejeo na zana pamoja na kununua mazao na kutoa mafunzo kwa wakulima.

10. Kuimarisha huduma za Ugani

Ili kuimarisha huduma za ugani nchini, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika imeshatekeleza yafuatayo:-

- Imefanya tathmini ya kina kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma za ugani nchini na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya kuimarisha huduma hizo ikiwemo kuajiri Maafisa Ugani, kuwapatia vitendea kazi, kuwapatia mafunzo, kujenga vituo vya taaluma katika ngazi za kata na kuwasilisha Serikalini na kukubaliwa kwa utekelezaji;
- Shilingi bilioni 17.266 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2007/2008 kwa ajili kuziwezesha Halmashauri kuimarisha uwezo wake wa

kuwahudumia wakulima kwa ufanisi zaidi ikiwemo kuwapatia Maofisa Ugani vitendea kazi. Hadi mwezi wa Desemba, 2007 jumla ya Shilingi bilioni 6.241 zilikuwa zimetolewa kugharamia kazi hiyo. Baadhi ya huduma hizo ni ununuzi wa vitendea kazi pamoja na baiskeli na pikipiki, ukarabati wa ofisi, ziara za mafunzo za wataalam wa ugani;

– Hadi mwezi wa Desemba, 2007, jumla ya Mashamba Darasa 1,091 yenye jumla ya wakulima takriban 40,000 yameazishwa katika mikoa yote nchini na yanatumika kuwafundisha wakulima kanuni za kilimo bora cha mazao. Aidha, jumla ya Wataalam wa Ugani 690 wamepatiwa mafunzo ya kuanzisha na kuendesha Shamba Darasa na wameanza kuwahudumia wakulima;

11. Kupanua Mafunzo ya Kilimo

Ili mpango wa kuimarisha huduma za ugani uwe endelevu, inabidi kutoa mafunzo na kuajiri wataalam wa Kilimo wa kutosha katika ngazi ya Tarafa, Kata na Kijiji. Wataalam hao watatakiwa kutoka kwenye vyuo mbalimbali vya mafunzo ya Kilimo. Wizara imefanya yafuatayo;

- Kuongeza vyuo vinavyotoa mafunzo ya Kilimo kutoka 7 hadi kufikia 11. Vyuo vilivyoongezwa ni Igabiro – Muleba, Chuo cha Taifa cha Sukari – Kidatu, KATRIN – Ifakara na KATC – Moshi.
- Kujenga na kukarabati madarasa, mabweni na nyumba za wakufunzi.
- Kuajiri wakufunzi 89 wa vyuo vya Kilimo kati ya 141 wanaotarajiwa kuajiriwa mwaka 2007/2008. Lengo ni kuajiri wakufunzi 258 ifikapo mwaka 2010/2011;
- Kununua vifaa vya mafunzo ya Kilimo;
- Wakufunzi 1,436 wanapatiwa mafunzo katika vyuo vya Kilimo ili kuandaa wataalam wenye sifa ya kuajiriwa katika mwaka 2008/2009. Lengo la idadi ya wakurufunzi 3000 haikufikiwa kutokana na kukosekana waombaji wa kidato cha sita wenye sifa. Ili kuziba pengo hili, Wizara sasa itachukua vijana waliomaliza kidato cha nne kwa mafunzo ya kilimo.

12. Kuimarisha Huduma za Utafiti

Ili kupata teknolojia sahihi zinazokidhi mahitaji ya Kilimo na kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za utafiti kwa:

- Kukarabati ofisi, nyumba za kuishi watumishi na mifumo ya maji imeanza kukarabatiwa katika vituo 6 vya utafiti ambavyo ni: HORTI Tengeru, Selian, Ukiriguru, Naliendele, Tumbi na Makutupora.

- Kununua vifaa vya maabara na ofisi pamoja na vitendea kazi (magari na kompyuta) kwa vituo vyote vya utafiti.
- Watafiti 50 wanaendelea kufadhiliwa katika mafunzo ya muda mrefu (Shahada za juu – MSc na PhD) katika vyuo vikuu mbali mbali nchini na nje ya nchi.

Mafanikio yaliyokwisha patikana kati ya Januari 2006 na Desemba 2007 ni pamoja na yafuatayo:

- Vituo vya Utafiti wa Kilimo vimetoa mbegu bora 26 za mazao mbali mbali ya chakula, mboga na biashara. Mbegu zina sifa nzuri za kutoa mavuno mengi, kustahimili ukame, ukinzani dhidi ya magonjwa, kukomaa haraka na kupendwa na walaji ukilinganisha na mbegu zilizopo. Mbegu hizo ni:- **Mahindi** – Vumilia H_1 na Vumilia $K_{1;}$ **Ngano** – Lumbesa; **Maharage** – Cheupe na Selian 06; **Ufuta** – Lindi 02; **Nyanya** – Meru; **Zabibu** – Makutupora Red na Chenin Nyeupe; na **Korosho** – aina mbali mbali 17.
- Matayarisho ya ramani za udongo na za mazao yanayoweza kustawi katika kanda za Kilimo kwa kila wilaya zimekamilika na kusambazwa katika wilaya zote.

13. Pembejeo na Zana za Kilimo

Mbolea

- Makisio ya mahitaji ya mbolea ni tani 385,000 kwa mwaka;

  Matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 77,557 kabla ya kurejesha mpango wa ruzuku mwaka 2003/2004 hadi tani 146,081 mwaka 2006/2007;

Serikali imepanga kutoa ruzuku kwenye mbolea jumla ya tani 91,324 mwaka 2007/2008. Hadi tarehe 3/1/2008 tani 44,412.85 (sawa na asilimia 49 ya lengo) zimefikishwa kwenye vituo vikuu 23 vya kusambazia mbolea. Kiasi cha tani 23,383.22 zimesambazwa kwa wakulima.

Mbegu Bora

- Makisio ya mahitaji ya mbegu bora ni tani 120,000 kwa mwaka.
- Kiasi cha mbegu bora kilichopatikana nchini kimeongezeka kutoka tani 10,477.17 mwaka 2005/2006 hadi tani 16,525.81 mwaka 2006/2007.
- Kwa mwaka wa 2007/2008 serikali imepanga kufidia tani 1,769.68 za mbegu bora kwa mpango wa ruzuku.

- Hadi tarehe 4/1/2008 tani 786.72, sawa na asilimia 44.5 ya lengo, zilifikishwa kwenye vituo vikuu 21 vya kusambazia mbegu bora. Tani 251.319 zimesambazwa kwa wakulima.
- Maandalizi ya kuzalisha miche ya chai 7,400,000 kupitia, Halmashauri za Wilaya, vikundi vya wakulima 110 na Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai yanaendelea. Hadi mwishoni mwa mwezi wa Desemba, 2007, miche ya chai 510,300 itakayotosheleza hekta 54.3 imezalishwa.
- Maandalizi ya kuzalisha miche bora ya kahawa 10,200,000 itakayotosheleza hekta 5,508 yanaendelea kupitia vikundi vya wakulima 400, Halmashauri za Wilaya, wakulima binafsi na TaCRI.

Wizara kwa kushirikiana na *Rockfeller Foundation na Bill and Melinda Gates Foundation* imeanza maandalizi yafuatayo;

- Kuandaa mawakala wa pembejeo za kilimo vijijini *(rural agro-dealers)* kwa kuwapa mafunzo na kuwawezesha kupata mikopo ili kupitia kwao, pembejeo ziweze kuwafikia wakulima. Kazi hii imeanza kwa mikoa ya Mbeya, Morogoro na Arusha.
- Kusaidia uzalishaji wa mbegu bora za aina mbalimbali *(seed multiplication)* ili ziwepo mbegu za kutosha kwa ajili ya wakulima;
- Kuyawezesha makampuni kusambaza mbolea, mbegu na madawa hadi vijijini kulingana na mahitaji ya pembejeo hizo hapa nchini;
- Kuanzisha utaratibu wa kutumia vocha katika kutoa ruzuku ya pembejeo ili ruzuku iweze kutolewa moja kwa moja kwa wakulima wenyewe.;

14. Matumizi ya Ardhi ya Kilimo

Wizara imefanya yafuatayo:

- Kuandaa mapendekezo ya sheria itakayotambua, kuainisha, kutenga na kulinda ardhi ya kilimo ili isimamiwe vizuri zaidi ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye;
- Kuandaa Mpango Kabambe wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo utakaokuwa dira ya upangaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kilimo nchini.
- Kutathmini na kuboresha takwimu za ardhi ya kilimo kwa ajili ya uwekezaji kama ilivyoainishwa kwenye taarifa ya Hazina ya Taifa ya Ardhi na kubaini maeneo mengine mapya katika wilaya 25 za mikoa saba ambayo ni Tanga, Dodoma, Morogoro, Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma.
- Kutoa mafunzo ya vitendo juu ya mbinu na teknolojia mbalimbali za matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na hifadhi ya vyanzo vya maji kwenye kanda za umwagiliaji za Mbeya, Morogoro, Kilimanjaro, na Manyara.

15. Matumizi ya Zana bora za Kilimo

Wizara imeendelea kuhimiza matumizi ya zana bora nchini ili kuongeza tija katika kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi. Hadi sasa, eneo linalolimwa kwa matrekta ni asilimia 10 tu. Matumizi ya wanyamakazi ni asilimia 20 na jembe la mkono asilimia 70. Matumizi ya zana bora bado ni duni kwani majembe ya mkono ni milioni 14, majembe yanayokokotwa na wanyamakazi 585,000, wanyamakazi 1,300,000 na matrekta 7,200 yanatumika nchini. Mahitaji kwa mwaka ni matrekta 1,500 na majembe ya wanyamakazi ni 40,000. Kwa sasa Serikali imetayarisha utaratibu wa kuwezesha makampuni binafsi kuingiza matrekta 1000 kila mwaka katika kipindi cha miaka minne.

Katika kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya nne:-

- Jumla ya Matrekta makubwa 464 na matrekta madogo 325 yameingizwa nchini na sekta binafsi.
- Matumizi ya matrekta madogo ya mkono yamekuwa na mafanikio makubwa hasa kwa wakulima wadogo katika kilimo cha mpunga katika mikoa ya Mbeya na Kilimanjaro. Hali hii imetokana na juhudi za makusudi za Wizara kutoa mafunzo na kufanya maonesho ya matumizi ya matrekta hayo madogo kwa wakulima katika mikoa yote 21.
- Vituo 12 vya kuendesha mafunzo ya wanyamakazi vimekarabatiwa na kupatiwa zana za mafunzo kwa ajili ya kufundisha wakulima. Ukarabati huu umeongeza idadi ya vituo vilivyokarabatiwa kufikia 55.
- Maafisa ugani 456 na wakulima wakufunzi 816 wamefundishwa katika vituo vya wanyamakazi ili waweze kutoa mafunzo kwa wakulima vijijini.
- Ili kuendeleza kilimo chenye tija cha kutumia zana na kupunguza uharibifu wa ardhi Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa ugani 300 ya kutumia zana bora za kilimo hifadhi.

16. Mikopo ya Pembejeo na Zana za Kilimo

Mfuko wa Pembejeo

Katika kipindi cha mwaka wa 2006/2007, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo kwa ajili ya kununulia pembejeo na zana bora zenye thamani ya shilingi bilioni 5.8.

Mikopo iliyokwishatolewa

Aina ya Mkopo	Idadi	Kiasi cha Fedha
Matrekta Makubwa	93	2,738,839,119.00
Pembejeo		2,814,870,800.00
Matrekta madogo	54	262,500,000.00
Kukarabati Matrekta	5	17,425,000.00
JUMLA		**5,833,634,919**

17. Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea

Kuanzia Januari, 2006 hadi Desemba, 2007 Wizara kwa kushirikiana na serikali za mitaa na wakulima imeendelea kupambana na milipuko ya visumbufu mbalimbali vya mimea na mazao ikiwa ni pamoja na:-

- Kudhibiti milipuko ya panya katika wilaya 19 nchini katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Tabora, Shinyanga, Tanga, Pwani, Morogoro na Mbeya ambapo jumla ya tani 878.44 za chambo chenye sumu zilitumika katika kudhibiti panya hao.
- Kutoa mafunzo endelevu juu ya udhibiti wa panya kwa wakulima 57,625.
- Kudhibiti ndege waharibifu wa nafaka katika Mikoa ya Morogoro, Tabora, Kilimanjaro, Dodoma, Shinyanga, Singida, Mwanza, Mbeya na Arusha ambapo zaidi ya ndege milioni 348.82 waliangamizwa na lita 8,084 za viuatilifu zilitumika.
- Kukarabati mitego 93 ya kutabiri milipuko ya viwavijeshi pamoja na kuwekwa mingine mipya 150 chini ya mradi wa udhibiti viwavijeshi shirikishi.
- Kutoa mafunzo juu ya udhibiti viwavijeshi kwa mabwana shamba 341 wakulima 233 na wahudumu wa mitego 43 katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Dodoma.
- Kudhibiti nzige wekundu katika maeneo ya mazalio yao ambayo ni mbuga za Wembere, Malagarasi, Iku/Katavi, Ziwa Rukwa na Bahi. Nzige hawa walikuwa kwenye eneo lenye jumla ya hekta 13,980. Jumla ya lita 6,390 za kiuatilifu zilitumika katika kudhibiti nzige hawa. Kazi hii imefanyika kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige Wekundu la Kusini mwa Afrika na Kati.
- Katika jitihada za kupambana na tatizo la inzi wa matunda Wizara imesambaza mitego 1,500 yenye kiuatilifu cha kudhibiti inzi hao katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani na wakulima wa AMAGRO *(Association of Mango Growers)* waliopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga.
- Ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nchini ulifanyika katika bandari za DSM, Tanga, Kigoma na Mtwara; viwanja vya ndege vya DSM na Kilimanjaro; vituo vya mpakani vya Namanga, Sirari, Horohoro, Murongo, Mutukula, Tunduma na Holili. Jumla ya tani 315,439.19 za mazao mbalimbali ya kilimo yalisafirishwa nje ya nchi na tani 210,480 za mazao yaliyoingia nchini yalikaguliwa na kupasishwa. Jumla ya Shs. 1,179,593,441.62 zilikusanywa.
- Katika jitihada za kupambana kudhibiti gugumaji, mbawakavu wameendelea kuzalishwa na kusambazwa ziwa Victoria pamoja na mabwawa yenye gugumaji.
- Katika jitihada za kudhibiti ugonjwa wa mnyauko wa migomba unaotishia zao la migomba katika mikoa ya Kagera na Mara wananchi wameendelea kuelimishwa na kuhimizwa kung'oa migomba yote iliyoathirika ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo kwenye maeneo mengine.

18. Uendelezaji wa kilimo cha Umwagiliaji

Tanzania ina eneo la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya hizo,

- hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kuendelezwa,
- hekta milioni 4.8 zina uwezekano wa kati wa kuendelezwa; na
- hekta milioni 22.3 zina uwezekano mdogo wa kuendelezwa.

  - Kati ya mwaka 2005/2006 na 2006/2007, jumla ya skimu 111 za umwagiliaji maji mashambani zenye eneo la hekta 23,953 ziliendelezwa na hivyo kufanya eneo linalomwagiliwa kuwa hekta 273,945 sawa na asilimia 11.9 ya eneo lote lenye uwezekano mkubwa kuendelezwa.
  - Katika mwaka 2007/2008, Wizara imepanga kuendeleza jumla ya hekta 20,515 ambapo hadi Desemba 2007 hekta 5,321 zimeendelezwa.
  - Mabwawa 10 yenye hekta 10,150 yanaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu.
- Wizara imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa eneo la hekta 125,579 katika sehemu mbalimbali nchini ambapo hadi Desemba 2007 eneo lililotekelezwa ni hekta 51,568.
- Katika ngazi ya wilaya, utekelezaji unafanyika kwenye miradi midogo yenye jumla ya hekta 16,150 chini ya Mipango ya Kuendeleza Kilimo ya Wilaya (DADPs). Skimu hizi ni zile ambazo zimeibuliwa na wakulima wenyewe.
- Katika ngazi ya Taifa utekelezaji unafanyika kwenye skimu zenye jumla ya hekta 4,365 ambazo utekelezaji wake unahitaji fedha nyingi kuliko zinazopatikana kupitia DADPs.
- Wizara inaendelea na uhamasishaji wa wakulima kutumia tekinolojia mbalimbali kama vile umwagiliaji maji kwa njia ya matone, matumizi ya pampu za kusukuma maji zinazotumia nishati ya mionzi ya jua, upepo, na diseli. Mashamba madogo ya mfano ya umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation*) yenye jumla ya hekta 235 yameanzishwa katika wilaya za Ilemela, Nyamagana, Magu, Bukoba Vijijini, Maswa na Tarime.

19. Kuimarisha na Kuendeleza Ushirika

Kufuatia kuwepo kwa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 yenye lengo la kupambana na kuondoa matatizo sugu yanayokabili ushirika nchini na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003, serikali iliridhia utekelezaji wa mpango mkakati wa mageuzi ya ushirika wa miaka 10 kuanzia mwaka 2005 mpaka 2015 unaojulikana rasmi kama '**Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika**'. Utekelezaji wa Programu hiyo katika kipindi cha 2005 mpaka 2007 umejumuisha mambo mbali mbali kama inavyoelezwa kwa kifupi hapa chini;

- **Upatikanaji wa viongozi bora:** uchaguzi wa viongozi wapya kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu ambavyo vipo hai umekamilishwa nchi nzima. Lengo la uchaguzi huo ni kupata viongozi waadilifu na wenye upeo katika masuala ya uongozi na biashara za kiushirika.
- **Mafunzo kwa viongozi waliochaguliwa:** mafunzo ya uongozi bora na uwajibikaji yametolewa kwa viongozi wa ushirika waliochaguliwa katika vyama vikuu na baadhi ya vyama vya msingi katika maeneo/mikoa ya kilimo cha korosho, pamba, kahawa na tumbaku.
- **Kuandaa na kutawanya miongozo:** Wizara imeandaa miongozo ya uhasibu, menejimenti ya fedha, mifumo ya taarifa za uendeshaji (MIS) na ukaguzi wa SACCOS ili kuviwezesha vyama hivyo kujiendesha kwa faida na kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na kujali maslahi ya wanachama wake.
- **Kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS):** kazi hii imefanyika katika maeneo yote ya nchi na pia viongozi wa siasa na serikali wameshiriki kwa kiasi kikubwa katika kazi hii. Matokeo ni kwamba idadi ya SACCOS imeongezeka kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi 4,428 mwaka 2007. Aidha, wanachama katika SACCOS hizo waliongezeka kutoka 255,938 (wanaume 169,989 na wanawake 85,949) hadi 764,602 (wanaume 494,946 na wanawake 238,135).
- **Kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga kwenye vyama vya ushirika:** Juhudi zinaendelea kufanyika kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga kwenye vyama vya ushirika vya aina mbalimbali (akiba na mikopo, kilimo, nyumba, umwagiliaji, mifugo, uvuvi, n.k.). Wanachama wa ushirika wameogezeka kutoka 750,000 mwaka 2005 mpaka 1,650,000 mwishoni mwa mwaka wa 2007.
- **Kuwezesha vyama vya ushirika kufanya maboresho na kukopesheka**: Serikali inaendelea kutekeleza ahadi yake ya kuvipunguzia vyama vya ushirika mzigo wa madeni ili viweze kufanya maboresho yanayohitajika na vilevile kuweza kukopesheka kwenye mabenki ya biashara. Kupitia utaratibu huo vyama vya ushirika vilivyokopa CRDB, EXIM na MUCOBA (na madeni yao ya mpaka Desemba 2004 kuhakikiwa na kukubaliwa) vimelipiwa jumla ya Shilingi bilioni 2.975 katika kipindi cha Oktoba/Novemba mwaka jana. Hali hiyo imewezesha benki ya CRDB kuvikopesha vyama vikuu vya ushirika maeneo ya korosho takriban shilingi bilioni 10 katika msimu wa 2007/2008 kwa ajili ya ununuzi wa korosho kutoka kwa wanachama wao.
- **Kuwezesha vyama vya ushirika kufanya biashara ya tija:** Wizara imesimamia shughuli ya ununuzi wa korosho za wakulima katika msimu wa 2007/2008 kwa madhumuni ya kuthibiti dhuluma ya bei waliyokuwa wanafanyia wakulima na baaadhi ya wanunuzi. Katika mkoa wa Mtwara umetumika utaratibu wa stakabadhi ghalani kupitia vyama vya ushirika vya msingi. Katika mikoa ya Lindi, Ruvuma (Tunduru), Pwani na Dar-es-Salaam ununuzi unafanywa kwa kupitia vyama vya ushirika vikuu. Mpaka Desemba 2007, tani 70,406 za korosho zilikuwa zimenunuliwa kutoka kwa wakulima

(kati ya 120 elfu zilizotegemewa kuzalishwa). Tani 50,430 kati ya hizo ni zile zilizonunuliwa katika mkoa wa Mtwara. Kupitia usimamamizi huo wakulima wanalipwa shilingi 610 kwa kilo ya korosho ya daraja la kwanza na shilingi 488 kwa kilo ya korosho ya daraja la pili. Maboresho ya biashara za kiushirika yatafanyika pia katika maeneo ya pamba na tumbaku katika msimu wa 2008/2009.

- **Utoaji wa mafunzo ya jumla ya ushirika na biashara:** Katika kipindi cha 2005 mpaka 2007, Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara (MUCCoBS) kiliendelea kutoa mafunzo kwa watendaji mbalimbali wa ushirika (baadhi yao wakiwa wamepata udhamini wa moja kwa moja wa Wizara) katika ngazi ya Cheti, Stashahada na shahada. Katika mwaka wa 2007 wanafunzi 61 waliokuwa chini ya ufadhili wa Wizara walihitimu kama ifuatavyo; stashahada ya uzamili (PGD), 10; stashahada ya juu (ADC), 39; na stashahada ya kawaida 12. Aidha wanafunzi 43 wanaendelea na kozi mbalimbali kwenye chuo hicho wakiwemo 35 kozi ya cheti (cha Micro-finance), 2 shahada ya kwanza (BA), 4 stashahada ya uzamili na 2 stashahada ya kawaida.
- **Kuimarisha usimamaizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika**: Wizara imeendelea kuwawezesha Maafisa Ushirika ngazi ya Halmashauri kuwa na uwezo wa kukagua vyama vya ushirika mara kwa mara. Hiyo ni pamoja na baadhi kupatiwa mafunzo stahiki na pia vitendea kazi (mathalan piki-piki kati ya 10 na 20 kila mwaka). Aidha Wizara imeendelea kuliwezesha Shirika la Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kuimarisha ukaguzi wa vyama wa mwisho wa mwaka. Katika mwaka wa 2006 COASCO iliweza kukamilisha kaguzi za vyama 1,973 na katika mwaka wa 2007 vyama 1,654 vilikaguliwa.

20. Hali ya Chakula nchini

Mazao ya chakula

Kwa ujumla hali ya chakula nchini katika mwaka 2007/2008 inatazamiwa kuwa nzuri. Tathmini ya uzalishaji wa mazao ya chakula mwezi desemba, 2007 imeonyesha kuwa uzalishaji utakuwa tani milioni 10.66 zikiwemo tani milioni 5.85 za mazao ya nafaka na tani milioni 5.17 za chakula. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2007/2008 yatafikia tani milioni 10.09. Kwa hiyo, inatarajiwa kuwa Taifa litajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 106.

Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imefanya tathmini ya hali ya chakula katika maeneo yenye upungufu wa chakula na kubaini kuwa jumla ya watu 214,135 wana upungufu wa chakula. Serikali imetenga jumla ya tani 5,139 za chakula.

21. Hifadhi ya Chakula ya Taifa

Kwa kutambua umuhimu wa tahadhari ya kujiandaa kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza wakati wowote, Serikali imeimarisha akiba yake ya chakula (SGR) kwa kununua mahindi na mtama. Hadi tarehe 02 Januari, 2008 SGR

ilikuwa na jumla ya tani 134,924 za mahindi na tani 7,214 za mtama kwenye maghala yake.

22. Uzalishaji wa Mazao makuu ya Biashara

Kwa muhtasari, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara kati ya mwaka 2005/2006 na 2006/2007 ulikuwa kama ifuatavyo:

- Uzalishaji wa kahawa uliongezeka kutoka tani 34,334 hadi tani 48,869;
- Uzalishaji wa tumbaku uliongezeka kutoka tani 56,463 hadi tani 65,299;
- Uzalishaji wa chai uliongezeka kutoka tani 30,000 hadi tani 34,446;
- Uzalishaji wa mkonge uliongezeka kutoka tani 27,794 hadi tani 30,934; na
- Uzalishaji wa korosho uliongezeka kutoka tani 77,158 hadi tani 92,232.
- Uzalishaji wa sukari ulishuka kutoka 263,317 hadi 192,535 kutokana ukame;
- Uzalishaji wa pamba ulishuka kutoka 376,591 hadi tani 130,565 kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa;
- Pareto kutoka tani 2,800 hadi 1,500 kutokana na kung'oa miche ya zamani na kupanda miche bora yenye tija kubwa na kiasi kikubwa cha sumu.

23. Mazao mapya ya biashara

Mazao ya Mboga na Matunda

- Mazao hayo ni pamoja na mboga, matunda, viungo, maua ambayo yameanza kupata soko la uhakika zaidi hususan katika nchi za Asia na Ulaya.
- Uzalishaji wa mazao hayo mwaka 2006/2007 ulikuwa kama ifutavyo mboga tani milioni 1.5; matunda tani milioni 1.7; viungo tani 85,000; maua tani 10,000.
- Mauzo ya mazao hayo yanaliingizia Taifa dola za Kimarekani milioni 147 kwa mwaka.
- Wizara inashirikiana na sekta binafsi kama Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani (*Horticulture Development Council of Tanzania* – HODECT) na Chama cha Wakulima wa Maembe (*Association of Mango Growers*- AMAGRO) kuendeleza mazao hayo.

Zao la Muhogo

Ili kuendeleza zao la muhogo kuwa zao la biashara, Wizara imejiwekea utaratibu wa kuzalisha vipando vya muhogo kwa wingi na kwa uhakika zaidi kwa kufanya yafuatayo;

- Tangu mwaka 2004/2005, Wizara imeweka utaratibu wa kushirikisha Jeshi la Magereza kuzalisha vipando bora vya zao la mhogo kupita Magereza 23 ili kuwezesha upatikanaji endelevu wa vipando bora vya muhogo kwa wakulima;

- Tangu mwaka 2004/2005 hadi 2006/2007 zaidi ya vipando vya muhogo milioni 30.35 vimezalishwa katika Magereza hayo;
- Musimu 2007/2008 lengo ni kuzalisha vipando milioni 17.2

MIPANGO NA MIKAKATI YA KULETA MAPINDUZI YA KIJANI NCHINI

24. Malengo ya Kufikia Mapinduzi ya Kijani

- Kuongeza matumizi ya mbolea kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2009/2010 ili kufikia virutubisho vya wastani wa kilo 50 kwa hekta;
- Kuongeza matumizi ya mbegu bora kufikia tani 120,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2010;
- Kupanua kilimo cha umwagiliaji kufikia hekta milioni 1.0 ifikapo mwaka 2015;
- Kupanua kilimo cha matrekta kwa kuwezesha uingizwaji wa matrekta angalau 1,000 kwa mwaka;
- Kuendeleza na kusimamia ushirika;
- Kuimarisha huduma za ugani; na
- Kuimarisha huduma za mikopo ya kilimo.

25. CHANGAMOTO

Changamoto katika kuleta mapinduzi ya Kilimo ni;

- Kutafuta raslimali za kutosha kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo ili Sekta ya Kilimo ikue kwa wastani wa angalau asilimia 10 kwa mwaka ifikapo mwaka 2010;
- Kuimarisha huduma za ugani;
- Kupanua matumizi ya teknolojia bora za kisasa;
- Kuimarisha na kuendeleza ushirika;
- Kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu ya kilimo;
- Kujenga uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha kutotabilika kwa hali ya hewa.

Stephen M. Wasira (Mb.)
WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA